**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

Mkuu wa Shule: 0752820960

Makamu M/Shule:0753071135

Matron/Patron: 0620824774

Shule ya Sekondari Nyarubanda,

**S.L.P 77, KIGOMA.**

**Tarehe 11 Juni 2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NYARUBANDA, HALMASHAURI YA WILAYA KIGOMA, MKOA WA KIGOMA MWAKA 2023.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya ……....................

**2.** Shule ya Sekondari Nyarubanda ipo umbali wa Kilometa 48 kutoka makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya Kigoma, barabara ya Manyovu. Usafiri wa gari kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi, Nauli ni Shilingi 5,000.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14 Agosti 2023, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13 Agosti 2023. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 28 Agosti 2023.

**3. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**3.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni suruari rangi ya bluu bahari (sky blue) na nyeusi zenye linda na zisizobana.
ii. Mashati mawili meupe yenye mikono mirefu yasiyo na maandishi.
iii. Sare ya Michezo ni tracksut ya dark blue na tsht ya bluu.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeupe/nyeusi za shule;
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta la rangi ya dark blue
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) ni suruali ya rangi ya damu yam zee.
ix. Tai ya rangi nyeusi na bluu bahari(sky blue) moja kwa kila rangi
x. Tisheti (T-shirt) yenye nembo ya shule inapatikana shule kwa gharama nafuu.

**3.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 9 counterbook 3 Quire
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. Mwanafunzi aje na godoro lenye ukubwa w aft 2.5 kwa ft 6.
v. Mashuka Jozi 2 bluu, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi ya bluu
vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Kwanja 1 (wanafunzi wa HGL), jembe 1 (wanafunzi wa HKL), reki 1(wanafunzi wa HGK), mifagio 2 wa ndani na nje kwa wanafunzi wote.

**3.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha zote zilipwe kwenye akaunti ya shule, JINA: **NYARUBANDA SECONDARY SCHOOL**, acc No, NMB **51601100023**. Mwanafunzi aje na risiti ya malipo. Pia mwanafunzi aje na BIMA YA AFYA.

## 4. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**5. Viambatisho na Fomu Muhimu (tafadhari vijazwe kwa ukamilifu)**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali (ukurasa wa 8 wa fomu hii)
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai (ukurasa wa 6 wa fomu hii)
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule (ukurasa wa 7 wa fomu hii)
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu (zibandikwe ukurasa wa 6 wa fomu hii)

6. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**


*Sylivanus Mataro*
**MKUU WA SHULE**

The Headmaster
Nyarubanda Secondary School
P. O. Box 77
Kigoma

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:-**

1. **MKUU WA SHULE: 0752820960**
2. **MAKAMU MKUU WA SHULE : 0753071135**
3. **PATRON: 0620593135**
4. **MWALIMU WA AFYA: 0767754039**

Rangi ya kitambaa cha suruali cha bluu bahari (sky blue)





CamScanner

**SHULE YA SEKONDARI NYARUBANDA**

**S.L.P 77**

**KIGOMA**

**FOMU NAMBA 1**

**HISTORIA YA MWANAFUNZI**

1. Jina la mwanafunzi …………………………………………………………………………
2. Jina la baba ……………………………………………………………………………..…
3. Jina la mama …………………………………………………………………………...
4. Jina kamili la Mlezi……………………………………………………………………….
5. Anuani ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………………………...
6. Uhusiano wa Mlezi …………………………………………………………………………
7. Kazi ya baba (mkulima, mfanyabiashara, mfanyakazi) ……………………………...
8. Kama ni mkulima zao muhimu analolitegemea ni ……………………………………...
9. Kama ni mfanyabiashara, biashara yake ni ……………………………………………
10. Kama ni mfanyakazi, kazi yake ni ……………………………………………………...
11. Afya ya mwanafunzi; kama anayo matatizo ya kiafya na hivyo kustahili huduma maalum, tafadhali mzazi/mlezi aeleze wazi …………………………………………
    ………………………………………………………………………………………………
12. Madhebu ya dini ……………………………………………………………………………
13. Jamaa na ndugu wanaruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa ruhusa ya mzazi/mlezi

| Jina kamili | Kazi yake | Namba ya simu | Picha |
|---|---|---|---|
| (a) …………………………………… | ……………………… | …………………….. | Bandika picha |
| (b) …………………………………… | ………………………. | …………………… | Bandika picha |
| (c) ………………………………….. | ……………………… | ……………………… | Bandika picha |
| (d) ………………………………… | ………………………. | …………………….. | Bandika picha |

**SHULE YA SEKONDARI NYARUBANDA**

**S.L.P 77**

**KIGOMA**

**FOMU NAMBA 2**

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE**

Jina la mwanafunzi …………………………………………………………………….
Jina mzazi/mlezi ……………………………………………………………………….
Anuani la mzazi/mlezi ………………………………………………………………..
Uhusiano ……………………………………………… (mjomba, shangazi, kaka, dada)

Mimi ……………………………………………………………………….. .. nikiwa nimechaguliwa kuwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Nyarubanda naamini kuwa nimetunukiwa nafasi hiyo niliyopewa na umma wa Tanzania. Hivyo naahidi kuwa nitajibidisha kadri ya uwezo wangu wote katika kazi zote nitakazopewa hapa shuleni nje na ndani ya darasa na kwamba ninatambua malengo ya shule ni ufaulu wa daraja la kwanza na la pili tu ili kuleta ufanisi.

Ili kutimiza shabaha hiyo ninakubali na kuahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitafanya kazi kwa **BUSARA, JUHUDI YA HALI YA JUU KABISA NA KUTII** kwa viongozi wote wa shule pamoja na sheria nikiwa na maoni au malalamiko ninaahidi nitayafikisha panapohusika kwa njia na taratibu zinazokubalika.
Sahihi ya mwanafunzi …………………………. Tarehe ……………………

Mimi …………………………………………………………………………….. mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……………………………………………………………. Ninaahidi kuwa nitatimiza wajibu wangu kama mzazi/mlazi wa mtoto huyo kwa kushirikiana na shule.
Sahihi ya mzazi/mlezi ………………………………… Tarehe ……..……..….

**SHULE YA SEKONDARI NYARUBANDA**
**S.L.P 77 KIGOMA**
**FORM NUMBER 03**
**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To medical Officer I/C of …………………………………………………………………
Designated Hospital, P. O. Box ………………………………………………………..
Please examine the above named in full as to his/her physical and niental fitness for being able to pursue two years of secondary school education. The examination should include categories a-m.
In case of any acute or defect/disability in each category or sub-category, may render the aspirant ineligible of admission or eligible of admission to schools of students with special needs.

(a) Pupil's name …………………………………………………………………
(b) Age …………………………………………………………..……………….
(c) Stool test ………………………………………………………………..
(d) Blood group …………………………………………………………………
(e) Urine analysis ………………..……………………………………………
(f) Sphills test …………………………………………………………………..
(g) Chest test …………………………………………………………………
(h) Speech ………………………………………………………………………….
(i) Eye test ……………………………………………………………………
(j) Abdomen …………………………………………………………………
(k) Chest X-ray …………………………………………………………………….
(l) Sickle cell test …………..………………………………………………
(m) WCB total Differential ……………………………………………………

Addition information and physical defect or impairment to pursue further studies
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

Signed by ……………………………………………………………………………….

Designation …………………………………………………………………………….

**Official Stamp**

**Date**